

Pambazuko

Toleo Namba 074

Jumatatu Juni 3-9, 2024

Tamisemi, Ardhi Mahakama vinara kukiuka maadili



Mohamed Mchengerwa
Waziri Tamisemi

Jaji Mkuu Prof.
Ibrahim Juma

Jerry Silaa -
Waziri Ardhi



Jicho la Tai

Kumbe kuna nyakati Makonda anapatia! UK. 5

Ruto, Gachagua wakaribia 'kuachana?' UK. 10

Bunge lagomea bajeti ya ziada UK. 14



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Ni wakati Rais Samia kukemea wanaoharibu

RAIS wa Tanzania Samia Suluhu Hassan anathibitisha kwamba anaweza kufanya vyema zaidi katika utendaji wake wa kazi ya kuongoza nchi, lakini huenda imani ya wananchi wake ikafifia ikiwa ataendelea kukaa kimya bila kukemea wenye kutaka “kumharibia.”

Wenye kutaka kumharibia Rais Samia wapo wengi; miongoni mwao ni watendaji wabovu katika ofisi za kutoa huduma kwa wananchi, hasa za serikali, halmashauri na kwenye taasisi za umma ambako wananchi wanapaswa kuhudumiwa vyema.

Katika ofisi nyingi za kutoa huduma kwa wananchi, sasa zimekuwa na watendaji wengi wa hovyo, wavivu, wanatumia muda na rasilimali za serikali kufanya mambo yao binafsi.

Pambazuko limepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao wanahoji – “kulikoni?” Kwamba nini kimetokea hadi watendaji waliokuwa na nidhamu ya kazi, kuwajibika, kujituma na kuhudumia vyema wateja wao- wananchi, sasa wamebadilika!

Mbali na kuwajibika ipasavyo, malalamiko hayo mengine yanadai kuwepo ongezeko la rushwa, kwamba watendaji wengi wa serikali sasa hawana woga wa kuomba rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Je, nani amewaambia kuwa Rais Samia ni mpole kiasi cha kufumbia ujinga huo wa kudai rushwa kana kwamba ni haki yao kabla ya kutoa huduma, tena nyingine zikiwa bure kabisa!

Wapo wanaoenda mbali zaidi na

kueleza kwamba huenda kauli ya Rais Samia kwamba “kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake,” umechukuliwa kama ruhusa ya kuikumbatia rushwa?

Sisi Pambazuko hatuamini kauli hiyo ya Rais Samia kama ilikuwa ni fursa ya kuruhusu watendaji wa serikali kuitumia kuomba rushwa.

Tunaamini tu kwamba wanaoichukua kauli hiyo kuwa ruksa, ni wale wenye hulka ya kukumbatia rushwa na kamwe siyo msukumo wa kauli hiyo unaowafanya kuomba rushwa kana kwamba ni haki yao ya msingi kabla ya kutoa huduma kwa wananchi.

Kikubwa ambacho Rais Samia anapaswa kujiepusha nacho, ni kuhakikisha kuwa wasaidizi wake anawafuatilia kwa karibu kwa kutumia vyombo vyake vingi; vya wazi na hata vile vya sirini ili kuhakikisha wote wenye lengo la “kumharibia” wanajulikana na kudhibitiwa mapema kabla madhara hayajawa makubwa na hata kuota mizizi.

Madhara ya watendaji wavivu na wala rushwa yanajulikana kwani huwakosesha wananchi haki zao za kupata huduma kutoka ofisi za serikali na kugeuza lawama zote kwa kiongozi wa nchi, ambaye sasa ni Rais Samia.

Kuwadhibiti wote wenye malengo mabaya, hata kama wao binafsi wanatajirika kwa rushwa na wizi mwingine, ni kazi inayopaswa kuimarishwa na kuwa endelevu ili kujenga Tanzania ambayo itakuwa nchi ya kupigiwa mfano kwa kutokuwa na rushwa na kuwepo kwa watendaji wa serikali wenye ufanisi mkubwa.

SAMIA AKIMTAZAMA SAMIA...



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia picha maarufu zenye taswira yake muda mfupi kabla ya kuanza kwa kikao maalum na wawekezaji na wamiliki wakubwa wa kampuni za Korea, wakati wa hafla ya chakula cha jioni kilichoandaliwa na wamiliki hao jana, huko Jiji la Seoul. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



"Pamoja na kuchelewa kwake kutendeka, uhuru wa habari lazima ulindwe kwa sheria badala ya utashi wa viongozi ili mtu yeyote yule alazimishwe kufuata sheria hiyo," - Simon Mkina, mhariri mwandamizi.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kuimarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

 Tigo
 Lipa kwa Simu
 Mpesa
 Airtel
 Holela

Kumbe kuna nyakati Makonda anapatia!

Na Igo AI

MZEE Tai leo kaamka kwa bashasha. Kapita kila nyumba ya jirani kusabahi na kukaribisha wenye nafasi wafike kwake kwa ajili ya kustaftahi.

Sura yake inaonekana dhahiri kwamba imevaa furaha isiyokuwa kifani. Tofauti na nyakati nyingine, leo kavalia shati lake la kijani – la mikono mirefu, yaani lile lenye rangi za chama chake.

Siyo shati tu la chama chake, kipiga pia suruali nyeusi, ambayo ni nadra mmo kuivaa hadi Februari 5 ya kila mwaka wakati wa maadhimisho ya kuzaliwa CCM yake.

Kadamka saa 12:37 hivi na “mdogomdogo” kapita kila nyumba jirani na baadaye kajongea kwenye meza ya magazeti na hapo kakusanya magazeti yote yanayosambazwa leo.

Wasaidizi wake wakiona hivyo, hupata fursa ya kuomba chochote wanachotaka kutoka kwa mstaafu huyo, ambaye amekunywa maji ya rangi ya bendera ya chama chake. Humwambii kitu kuhusu CCM.

Mzee Tai karejea nyumbani sasa na kumwambia msaidizi wake, aandae chai ya nguvu, kwani leo hataki kula magimbi kwa chai ya sturungi. Anahitaji mayai, tena Spanishi, bofelo lenye jamu kwa chai ya maziwa, ambayo haijaongezwa tone la maji.

Akiwa ameketi sebuleni akisubiri kustaftahi, Mzee Tai akamuita mwandishi wake na kuanza kumpa “matirio” ya kuandika ili Watanzania wasome mawazo yake kupitia gazeti analoliamini la Pambazuko.

“Sasa waambie hao watu wa Pambazuko, kwamba nimegundua kitu ambacho lazima watu wakitambue na ikiwezekana wafuatilie na kuweka kumbukumbu sahihi ili baadaye wapate jambo la kusema,” akasema Mzee Tai.

“Jambo langu ni dogo tu, ni kuhusu yule kijana aliyedai kwamba anakula raha zaidi duniani kuliko mtu yeyote,



Paulo Makonda, Mkuu wa mkoa wa Arusha

nimemsahau jina lake, ni yule alikuwa mkuu wa mkoa gani sijui,” je, unamkumbuka?”

Kabla hajakaa sasa, mwandishi wake akajibu: “Ahh Mzee Tai, huyo anaitwa Paulo Makonda, ni yule aliyedaiwa kuvamia Kituo cha Televisheni cha Clouds, yule aliyekuwa akitembea kwa baiskeli, mara kadandia punda, mara ngamia, mara akisukuma mkokoteni uliosheheni ndizi...mara...”

Mzee Tai akamkatiza mwandishi wake kwa maelezo kwamba hakutaka mambo mengi ya historia ya Paulo Makonda, bali alitaka jina lake tu ili aendelee na stori yake.

“Yaani wewe mwandishi unapenda sana kujidai unawafahamu watu na tabia zao, tena zile mbaya-mbaya ndiyo unapenda, wewe hujui watu wanabadilika...”

“... hivi unadhani Makonda wa sasa, huyu wa Arusha ndiyo yuleyule wa miaka saba au nane iliyopita, wewe mtu wa namna gani...”

“Huyu Makonda wa sasa anapatia, anakemea rushwa hadharani, na hata naamini katika kificho, hebu muache afanye kazi zake...” akamaliza Mzee Tai, huku akikaribishwa mezani kwa ajili ya chai.

Habari

Tamisemi, Ardhi, Mahakama vinara kukiuka maadili

Na Mwandishi WETU

KUKIUKWA kwa maadili ya kazi kwa baadhi ya watendaji wa serikali wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao, ni miongoni mwa malalamiko mengi ya wananchi.

Hii inathibitishwa na watendaji hao kuomba rushwa, kuiba muda wa kufanya kazi za mwajiri, uzembe na matumizi ya vifaa vya serikali kwa manufaa binafsi.

Ripoti ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliyotolewa hivi karibuni na Pambazuko kuona nakala yake, imeweka wazi kero ya maadili kwa watendaji wa serikali.

Bila kumung'unya maneno, ripoti hiyo imezitaja wizara mbili kuwa watendaji wake ni vinara wa kulalamikiwa na wananchi kwa kukiuka maadili katika utendaji wao wa kazi.

Wizara hizo ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), na ile ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mbali na wizara hizo, pia Idara ya Mahakama nayo imo.

Kwamba taasisi hizo tatu zimeongoza kwenye orodha ya taasisi zilizolalamikiwa na wananchi kuhusu kukiuka maadili kwa baadhi ya watendaji wake, wengi wakiwa viongozi kwa miaka miwili mfululizo; 2021/22 na 2022/23.

Pamoja na taasisi hizo, taasisi nyingine ambazo zinatengeza orodha ya taasisi kumi zinazolalamikiwa sana na wananchi kuhusu kukiuka maadili ni Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Afya, pamoja na Bunge.

“Kuna uwezekano kuwa Tamisemi inaongoza kulalamikiwa kwa sababu ndiyo taasisi yenye viongozi wengi ambao shughuli zao zinahusisha kukutana na wananchi moja kwa moja mara nyingi,” anasema Waziri Kipacha, Katibu wa



Rais Samila Suluhu Hassan

Ukuzaji wa Maadili katika Sekretarieti hiyo.

Pambazuko imebaini kuwa kulikuwa na ujumla ya malalamiko 120 dhidi ya taasisi hizi kumi mwaka 2021/22 na mwaka uliofuatia idadi ya malalamiko iliongezeka hadi 179.

Wakati Tamisemi ilipata malalamiko 63 mwaka 2021/22 mwaka uliofuatia malalamiko yaliongezeka hadi 93. Wizara ya Ardhi ilikuwa na malalamiko saba mwaka 2021/22 na mwaka 2022/23 ikapata malalamiko 16.

Kwa upande wake, Mahakama ilitolewa malalamiko matano mwaka 2021/22 huku mwaka uliofuatia malalamiko dhidi ya taasisi hiyo muhimu kwa utoaji haki na kutafsiri sheria, yakiiongezeka hadi 15.

Kibacha alibainisha kuwa Sekretarieti ya Maadili inakabiliwa na changamoto kubwa ya mwamko mdogo wa wananchi na taasisi nyingine kufikisha malalamiko yao dhidi ya maadili ya viongozi wa umma wanaokiuka maadili.

Licha ya malalamiko mengi katika jamii juu ya ukosefu wa maadili ya viongozi wa umma, lakini Kibacha alionyesha kuwa malalamiko yanayowasilishwa kwa Sekretarieti hayafikii 300 kwa mwaka.

Mathalani, alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mwaka ambao Sekretarieti ilipokea malalamiko

Tamisemi, Ardhi, Mahakama

Inatoka Uk. 6

mengi ni 2019/20 ambapo kulikuwa na malalamiko 234.

“Baada ya uchambuzi wa malalamiko hayo ni malalamiko 57 tu ndiyo yalikuwa na uzito wa kufanyiwa uchunguzi,” alisema na kuongeza:

“Pamoja na malalamiko yaliyopokelewa, uchunguzi uliyofanywa kwa kipindi cha miaka mitano, hasa malalamiko yanahusu sheria, yameendelea kuongezeka kwa maana ya kuongezeka kwa rasilimali kwa ajili ya kuchunguza ukiukwaji wa makosa ya kisheria.”

Kibacha alibainisha kuwa mwaka 2022/23 jumla ya viongozi tisa kutoka taasisi tano za umma walifikishwa katika Baraza la Maadili kujibu tuhumba mbalimbali dhidi nyao.

Viongozi hao walitoka Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) ikiwa na watuhumiwa wawili, Tacaids, Halmashauri ya Mji Mbulu na PSSF ambayo ilikuwa na watuhumiwa watatu.

Viongozi hao ambao walijumuisha wakurugenzi wakuu, wakurugenzi wa vitengo na mwenyekiti, walituhumiwa kwa makosa mbalimbali.

Makosa hayo ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka, kuweka shinikizo lisilofaa katika kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu na kuajiri pasipo kufuata taratibu, kujiingiza katika mgogoro wa kimaslahi, matumizi ya lugha chafu, matusi na vitisho, uonevu, vitisho vya kutumia silaha, matumizi ya rasilimali za umma kwa manufaa binafsi na kutozingatia sheria katika utendaji wao.

Baadhi ya wahariri wakizungumzia ripoti hiyo walionyesha kusikitishwa kwao na baadhi ya vipengele katika sheria ya maadili ya umma, hasa vile vinavyoleta usiri katika masuala ambayo kimsingi yalipaswa kuwekwa wazi.

Mhariri Pascal Mayala alisema kipengele cha sheria kutoa ruhusa kwa watu kuzipitia fomu za viongozi, lakini



Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma

wakikatazwa kusema chochote kuhusiana na kile wanachokiona kwenye fomu hizo, hakifai kwani kinaendekeza usiri, jambo ambalo halitakiwi katika mapambano dhidi ya utovu wa maadili miongoni mwa viongozi.

“Sasa inakuwa na maana gani mtu kuruhusiwa kuangalia fomu ya kiongozi, halafu akatazwe kusema hadharani jambo lolote kuhusiana na taarifa ambazo kiongozi husika amejaza kwenye fomu yake?” alihoji Mayala.

Mhariri Jesse Kwayu aliishauri sekretarieti kuanza kufanya ukaguzi wa mitindo ya maisha ya viongozi ambao wengi wanaonekana kuwa na maisha aghali kuliko vipato vyao vinavyofahamika.

“Ninapendekeza hili kwa sababu viongozi wengi sasa hivi wana maisha aghali ambayo hayaendani na vipato vyao. Ni vyema tujue wanapata wapi pesa za kuishi maisha haya katika nchi masikini kama Tanzania,” alisisitiza.

Wahariri hao pia walionyesha mshangao kwa sekretarieti kushindwa kuwachukulia hatua baadhi ya viongozi ambao kwa kauli au matendo yao, wamekuwa wakiwadhalilisha watumishi wa umma hadharani.

Waligusia kuhusu kuwepo kwa baadhi ya viongozi kuwa na kauli za kudhalilisha wanaowaongoza, wakati mwingine ikiwa hadharani.

Hata hivyo, Sekretarieti ilibainisha kuwa mengi ya matamshi hayo yanashughulikiwa na vyombo vingine vya kimaadili kama vile chama tawala ambako viongozi hao wanatoka.

Dhana Murua

Demokrasia ya kweli haina mapambio

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

TUNAPOANGALIA nguzo za msingi za demokrasia. Ni vyema kukumbuka kwamba demokrasia ni uwepo wa nguzo hizo zote katika madaraja mbalimbali ya utawala.

Nguzo hizi zinaweka kipimo cha kinadharia juu ya jinsi mambo yanavyotakiwa kuwa. Mfano, tungeweka ubao wa kutolea alama za kupima jinsi kila nguzo ilivyotimizwa katika kila taifa au taasisi, basi tungepata picha ya utekelezaji kidemokrasia.

Katika utawala wa taifa tulizungumzia mihimili mitatu ya serikali ambayo ni utawala, bunge na mahakama. Mihimili hiyo yaweza kuwepo, lakini katika utendaji isiwe na tija katika kuboresha maisha ya raia. Mihimili hiyo yaweza kuwa klabu za wenye nguvu za kukandamiza haki za raia.

Sifa pekee zinazoweza kuleta tofauti ni hizo nguzo za demokrasia. Nguzo za demokrasia ndio huongeza thamani ya utawala wowote. Ndizo hushikilia kwa sehemu kubwa dhana nzima ya utawala bora. Nguzo za demokrasia ndio hufafanua demokrasia yenyewe.

Tunapoutazama uongozi wowote na kufanyia tathmini kwa misingi ya nguzo hizo, ndipo tunaweza kuweka kiasi cha demokrasia katika taasisi yeyote.

Tunaweza kutumia kipimo cha kuanzia sifuri mpaka kumi. Sifuri hapo ni kipimo cha uongozi usiokidhi kigezo cha nguzo yeyote katika kiwango chochote. Hapa tunaona utawala wa kidikteta uliokithiri.

Ambapo alama kumi ni uongozi wa kufikirika ambao hutimiza vigezo vya nguzo zote pasipo upungufu wowote. Huu ni utawala wa kidemokrasia wa kiwango cha juu.

Tunapoangalia nguzo hizi ndani ya kila mhimili wa serikali, tunaweza kujiuliza maswali kadhaa, je, inawezekana mhimili



mmojawapo wa serikali (kwa mfano bunge) ukaongozwa kidemokrasia ambapo miwili mingine haiendeshwi hivyo? Je, mhimili mmoja au miwili inapokuwa ya kidemokrasia, serikali yote imepata sifa ya kuwa ya kidemokrasia?

Serikali huonekana kuwa ya kidemokrasia pale ambapo mihimili yote huendeshwa kidemokrasia. Demokrasia inatakiwa kuwa kama wimbi la bahari ambalo likipita hunyanyua juu mashua zote.

Tena ieleweke kwamba tunapozungumzia mihimili mitatu ya serikali hatuzungumzii serikali tatu, bali serikali moja katika mihimili mikiu mitatu ya utendaji. Huu ni mgawo wa wajibu kwa ajili ya utawala bora na utendaji wenye ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Kwa hiyo, ni muhimu nguzo hizo za demokrasia zionekane kama utandu wa buibui katika maisha na utendaji wa mihimili yote siku kwa siku.

Ni muhimu ziwepo katiba na sheria zenye nguvu ya kuonyesha hivyo na ambazo ni rahisi kusimamiwa na hatua kuchukuliwa kwa wanaoisigina.

Ilipo demokrasia yenye taji la nguzo hizo muhimu, hakuna haja ya kutafuta maneno ya kusifu watawala, bali uongozi wao bora utawapa sifa na heshima.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Umaruki waungwe mkono katika hili

Na Rashid MTAGALUKA

VIPO vyama na mashirika mengi yasiyo ya serikali hapa nchini ambayo kila moja limeundwa kwa malengo mahsusi waliyokubaliana wanachama kwa ujumla wake.

Viko vyama vya kuchangiana fedha (upatu) wakati wa sherehe na wakati wa misiba, kwenye ngazi mbalimbali kuanzia vitongoji, vijiji, mitaa na viko vyama vya aina hii katika ngazi ya mikoa.

Binafsi nimeshuhudia uwepo wa vyama hivi katika maeneo mbalimbali ambapo wanachama na wanaowahusu wamekuwa wakinufaika kwa kiasi kikubwa kila wanapopatwa na masaiibu au hata kuwa na kitu cha kuwafanya washareheke.

Ukiachilia mbali changamoto wanaozokumbananza viongozi wanaojitolea kufanya kazi na vyama hivi vya hiyari, lakini ukweli ni kwamba, ziko faida kubwa zinazopatikana kijamii na hata taifa letu kwa ujumla limekuwa likifaidika na uwepo wa vikundi hivi.

Kwa mfano Umoja wa Maendeleo wa Watu wa Rufiji, Pwani na Kilwa, Lindi waishio Morogoro waliojikusanya na kusajiliwa umoja wao serikalini kwa lengo la kusaidiana wao kwa wao, unaweza kutumika kama ushahidi wa maneno yangu.

Umoja huu unaofahamika kwa kifupi cha Umaruki, Alhamisi wiki iliyopita walikwenda Kibaha ziliko ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Pwani kukabidhi msaada wa marobota ya nguo za mitumba kwa watu walioathiriwa na mafuriko kwenye wilaya za Rufiji na Kibiti.

Kama nilivyotangulia kusema hapo juu, Umaruki ni chama cha kijamii chenye mchanganyiko wa wenyeji wa mikoa ya Pwani, Mtwara na Lindi wanaoishi mkoani Morogoro, walioamua kuutumia umoja wao kusaidia wenzao katika wilaya za Kibiti na Rufiji waliopata athari za



Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani Rashid Mchatta (mwenye tai) akipokea marobota ya nguo kutoka kwa viongozi wa Umaruki wiki iliyopita (Picha na Mpigapicha Wetu).

mafuriko.

Msaada wa marobota hayo ya nguo yenye thamani ya shilingi milioni saba na laki saba waliokabidhi kwa Katibu Tawala, Rashid Mchatta kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge umedhihirisha kwamba, vikundi vya namna hii ni muhimu kuendelea kuwepo kwenye jamii yetu.

Na siyo kuwepo tu, bali serikali kwa kutumia taasisi zake zinazoshughulika na vyama hivi vya hiyari, inapaswa kuviunga mkono kwa kuvijengea uwezo walau wa mafunzo kwa viongozi wake ili vifanye vyema zaidi akzi zao.

Najua inawezekana leo hii hoja yangu isieleweke vyema, lakini serikali ikionyesha kutambua mchango wa vikundi hivi vya kijamii kwa kuwasogezea elimu ya uongozi, itakuja kunishukuru baadaye.

Vyama kama Umaruki visiishie kutambulika serikalini kisheria tu, bali wenye mamlaka wanapaswa kwenda mbele zaidi kwa kuhakikisha vinaendelea kuwa hai ili wakati mwingine nchi inapokumbwa na majanga kama haya, vikundi hivi viweze kuona haja ya kusaidiana na serikali katika kupeleka misaada ya kiutu.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa Pambazuko anayepatikana kwa simu 0784 438546/mtagaluka@gmail.com

Kenya

Ruto, Gachagua wakaribia 'kuachana?'

Na Julius MKAMBI

‘KAMA mbaya mbaya...’ ndiyo ilikua kauli iliyotolewa na Gavana wa Kaunti ya Nyeri nchini Kenya, Mutahi Kahiga, akimkingia kifua Naibu Rais Rigathi Gachagua, kutokana na tetesi ya kuchipuka mtafaruku na bosi wake, Rais William Ruto.

Je, historia ndiyo inajirudia? Itakumbukwa katika muhula wake wa pili, Rais (mstaafu) Uhuru Kenyatta alitofautiana na Ruto wakati huo akiwa naibu ke, hali iliyosababisha Kenyatta kumuunga mkono hasimu wake kisiasa, Raila Odinga, kwenye uchaguzi mkuu uliopita.

Rais Ruto alisema hataruhusu kilichomtokea wakati ule, kimtoke naibu wake, hivyo akafikia uamuzi wa kuweka wazi majukumu ya Gachagua, lakini baadhi ya wanasiasa kutoka Mlima Kenya ambako anatoka naibu rais huyo, wamesikika wakinung’unika wakidai Ruto anamtega msaidizi wake.

Gavana Kahiga aliongoza baadhi ya wanasiasa kuwashutumu wenzao waliokaribu na Rais Ruto kwa kupanga na kusababisha sintofahamu kati ya Ruto na Gachagua wakidai ni ishara ya kuhakikisha Ruto anapata mgombea mwenza mwingine, Kenya itakapoelekea katika uchaguzi mkuu ujao mwaka 2027.

“Hakuna nafasi ya migawanyiko. Tutahakikisha Rais Ruto na naibu wake wanafaulu katika ajenda ya mabadiliko na kutimiza ahadi za kabla ya uchaguzi. Pia tuna matarajio kama jamii kuhusu mageuzi katika sekta ya kahawa, chai, ufugaji wa ng’ombe wa maziwa, parachichi na makadamia,” alisema Kahiga.

Tetesi za tofauti kati ya viongozi hao wawili wakuu serikalini zilishika kasi siku chache kabla Rais Ruto kwenda Marekani. Maswali yakiibuka kuhusu



Rais Ruto na naibu wake - Gachagua

aliko Gachagua baada ya kukosa kwenye hafla 11 kuu za serikali huku pia kukiwa na ukimya katika akaunti zake za mitandao ya kijamii ambazo kwa kawaida zimekuwa zikitoa taarifa za mara kwa mara.

Miongoni mwa hafla hizo ni kutokwepo kwake wakati Rais wa Uganda Yoweri Museveni alipofanya ziara ya siku tatu nchini Kenya kufuatia mwaliko wa Rais Ruto.

Gavana Kahiga ambaye ni mtetezi mkubwa wa Gachagua, alisema viongozi wa Mlima Kenya hawatakaa kimya na kutazama naibu rais akidhalilisha kama vile alivyofanyiwa Ruto alipokuwa akishika wadhifa huo kwenye serikali ya Kenyatta.

“Hatutaruhusu hili litokee, kama mbaya mbaya. Haitakuwa biashara kama kawaida. Hutamdhalilisha mtoto wetu tukiona,” alionya Kahiga.

Wanasiasa wanaomtetea Gachagua walidai timu ya viongozi vijana ndani ya muungano tawala wa Kenya Kwanza ndio wanaozua mtafaruku kati ya Ruto na naibu wake, kwa kushinikiza kile kinachoitwa mabadiliko ya kizazi kwa lengo la kutaka kuwaondoa viongozi wazee.

Hata hivyo, Ikulu kupitia msemaji wake, Hussein Mohammed ilipuuza madai ya kuzorota kwa uhusiano kati ya Rais Ruto na Naibu Rais Gachagua baada ya kuulizwa na Pambazuko.

Wabunge wampasha Jerry Silaa

Na Mwandishi WETU
Dodoma

UTARATIBU wa kunyang'anya umiliki wa ardhi na hata kufuta hati – unaofanywa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kwenye mikutano ya hadhara, umewakera wabunge.

Kutokana na mtindo huo wa uamuzi na kuchukua hatua, wabunge wamemuonya Silaa huku wakimtaka waziri huyo kufuata taratibu, kanuni na sheria katika utendaji wake.

Wabunge hao wamedai mtindo huo wa uongozi wa kuchukua uamuzi wa papo kwa papo ni njia nyepesi ya kujitafutia sifa za mitandao ya kijamii au kwenye vyombo vya habari.

Walitoa ushauri huo wiki iliyopita wakati wakijadili hotuba ya bajeti ya wizara hiyo bungeni, jijini Dodoma.

Watunzi hao wa sheria na kuisimamia serikali, wametoa ushauri huo katika kipindi hiki ambacho Silaa amekuwa na mvuto mkubwa kwenye vyombo vya habari hasa vya mtandaoni kutokana na jinsi anavyoshughulikia migogoro ya ardhi.

Wameonya kuwa umaarufu huo anaoupata sasa usimfanye avimbe kichwa na kusahau kuwa sekta anayoiongoza inasimamiwa na sheria, kanuni na taratibu.

Halima Mdee alimuonya waziri huyo kuwa asipokuwa makini anaweza kupotoshwa na watu wanaomzunguka.

Mbunge Mdee alisema kuwa kuna uwezekano mkubwa migogoro ya ardhi ambayo waziri anajichukulia umaarufu kwa kuitatua kwenye mikutano ya hadhara, ni migogoro ya kutengenezwa yenye maslahi kwa vigogo ndani ya wizara, serikalini au kwenye sekta binafsi.

Alisema upo uwezekano mkubwa kwamba migogoro ya ardhi haitatuliwi kwa wakati kutokana na ufinyu wa bajeti – kwani imekuwa ikipungua kila mwaka.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa

Akitoa mfano Mdee alisema kuwa katika mwaka wa fedha unaomalizika mwaka huu, bajeti ya matumizi mengineyo katika wizara hiyo ilikuwa ni shilingi bilioni 37.6, lakini katika mwaka ujao wa fedha imepunguzwa hadi shilingi bilioni 36.6.

Aidha, Mbunge huyo alibainisha kuwa bajeti ya maendeleo nayo imepunguzwa kutoka shilingi bilioni 82 katika bajeti inayofikia ukingoni, hadi shilingi bilioni 70 mwaka ujao wa fedha.

Alimtaka Silaa kuacha kulewa sifa anazozipata hivi sasa kwa jinsi anavyoshughulikia migogoro ya ardhi, kwani anachokifanya ni sawa na kutia tone la maji kwenye bahari iliyojaa papa - kwani migogoro ya ardhi ni mingi mno nchini.

“Wananchi wameonyesha wana imani na wewe mshemiwa waziri, katika masuala haya nikuombe usikilize wananchi, nenda kawasikilize wananchi. Usiwasikilize wapambe wanaokuzunguka, watakupotosha kwa sababu wana maslahi kwenye migogoro hii,” aliongeza Mdee.

Godwin Kunambi aliungana na Mdee katika mchango wake akimtaka Waziri Silaa kutengeneza mifumo mizuri kwani ndio itakayosaidia kuweka utaratibu ambao hautazalisha migogoro ya ardhi mingine.

Alimpa pole waziri huyo kwa sababu

Habari

Wabunge wampasha Jerry Silaa

Inatoka Uk. 11

amepewa sekta nyeti, lakini akinukuu vifungi vya Biblia alisema kuwa sekta hiyo imelaaniwa na Mungu.

Kunambi alisema licha ya ardhi kuwa rasilimali bora, bado haiisaidii nchi kwa sababu ya kukosekana kwa mifumo madhubuti ya kuhakikisha kuwa rasilimali hiyo inatumika ipasavyo.

Alisema inasikitisha kuwa serikali inarasimisha ardhi wakati ardhi hiyo bado haijapangwa wala kupimwa kama taratibu bora za matumizi ya rasilimali havyotaka.

“Utaratibu wa kupima ardhi unafanyika iwapo kuna nyaraka mbili zimepatikana ambazo ni mpango kabambe wa matumizi ya ardhi na mpango kapambe wa miundombinu,” alisema.

Kwa mujibu wa Kunambi, ili kufanya rasilimali ardhi iwe na manufaa kwa watumiaji, kuna hatua za kufuata ikiwamo upangaji wa matumizi, upimaji wa ardhi husika na baada ya hapo ndipo ardhi hiyo inarasimishwa.

“Sasa inashangaza kuwa serikali inarasimisha ardhi ambayo haijapangwa wala kupimwa, ukiondoa Dodoma sehemu nyingine zote hazina master plan. Dar es Salaam ni squatter city, Mwanza ni squatter city, Arusha ni squatter city,” alisema.

Aliitaka wizara hiyo kukaa pamoja na Wizara ya Tamisemi kutengeneza mpango wa pamoja wa matumizi ya ardhi na kila halmashauri nchini ielekezwe kuwa na mpango kabambe wa ardhi na miundombinu.

Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kagera, Conchesta Rwamlaza, alitishia “kuwakwida” watumishi wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma iwapo wataendelea kumzungusha kuhusu kiwanja alichokilipia tangu mwaka 2022, lakini hajapatiwa hati yake hadi leo licha ya kulifuatilia suala hilo kwa karibu.

Akizungumza kwa sauti yenye ukali bungeni, mbunge huyo alimtaka Silaa



Migogoro ya ardhi imekuwa kero kubwa nchini Tanzania, huku watendaji wa wizara wakilaumiwa kuwa chanzo chake. Hapa wanaonekana baadhi ya wapima ardhi wakionyesha ramani kwa wananchi. (Picha na mtandao).

kufanya haraka kushughulikia mgogoro wa kiwanja alichodai kutapeliwa huku akikaripia kwamba apewe hati yake - “kabla sijamkwida mtu.”

Alisema kuwa alipewa kiwanja hicho Juni 16, 2022 na kukilipia Juni 29, 2022 kupitia control number 992000375444 katika akaunti ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, “lakini katika kliniki iliyofanywa mwaka jana na Angelina Mabula (aliyekuwa Waziri wa Ardhi) nilishangaa kuwa kiwanja hicho hicho kilikuwa kimeuzwa kwa mtu mwingine ambaye naye alikilipia na kupewa hati tangu 2021,” alilalamika.

Rwamlaza alisema suala la umilikishaji pandikizi limekuwa sugu na kumtaka waziri kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

“Ukitaka kuona zahama nenda kitengo cha ardhi uone watu wanavyoteseka. Utaona jinsi gani kitengo hiki cha ardhi yaani sijui niwaiteje, mimi nawaita ni jini la pembe mia,” alisema na kuhoji: “Mimi ni muathirika, kama mbunge nafanyiwa hivi, je, watu wengine wa kawaida itakuwaje?”

Mbunge huyo alibainisha kuwa katika ufuatiliaji alielezwa kuwa nyaraka alizoziwasilishwa kwa ajili ya kupatiwa hati zimepotea.

Bunge lagomea bajeti ya ziada Utalii

Na Mwandishi WETU
Dodoma

BUNGE la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limekataa mpango wa matumizi ya fedha za bajeti ya ziada zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Sababu ya Bunge kukataa bajeti hiyo ya ziada ni kiasi kikubwa cha fedha kuelekezwa kwenye matumizi mengine badala ya miradi ya maendeleo.

Akiwasilisha bajeti ya wizara hiyo Jumaa iliyopita, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angela Kairuki, aliliambia Bunge kuwa serikali imeamua kuongeza bajeti ya wizara hiyo kwa kiasi cha shilingi bilioni 19.

Hata hivyo, katika taarifa yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, licha ya kueleza kufurahishwa na hatua hiyo ya serikali, ilipinga mpango ulioletwa na wizara hiyo kuhusu matumizi ya fedha hizo za ziada kwenye bajeti.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri Kairuki, kiasi cha shilingi bilioni tano tu, sawa na asilimia 26 ya ongezeko hilo, ndicho kitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo huku shilingi bilioni 14, sawa na asilimia 74 ya fedha hizo kikitengwa kwa ajili ya matumizi mengine – hasa ya uendeshaji wa wizara.

Ilikuwa ni matarajio ya kamati kuwa kiasi kikubwa cha fedha hizo zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ili kuleta tija zaidi na kuongeza makusanyo ya fedha, hasa za kigeni – kutokana na shughuli za utalii.

Akisoma taarifa ya kamati hiyo, mwenyekiti wake, Timetheo Mnzava alisema jambo hilo halikubaliki, hasa ukizingatia kuwa wizara ina matatizo mengi ambayo utatuzi wake unahitaji fedha.

“Kamati haikuridhishwa na mgawanyo



Waziri wa Maliasili na Utalii - Angela Kairuki

wa nyongeza hiyo kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni baadhi ya taasisi za wizara kutokuwa na ofisi, mzigo wa madeni, uchakavu wa miundombinu na wananchi kuvamiwa na wanyama wakali na waharibifu...

“... Hivyo, ni maoni ya kamati kwamba ongezeko hili halitakuwa na tija kwa wizara kwa sababu haliendi kushughulikia changamoto za msingi,” alisema Mnzava.

Mnzava alisema pamoja na kwamba taasisi zimeruhusiwa kukusanya asilimia sita na kuitumia kwenye utangazaji wa utalii, bado shilingi bilioni moja imeongezeka kwenye Idara ya Utalii kwenye utangazaji wa utalii, safari za nje, kubaini vivutio na mazao mapya ya utalii, utafiti kuhusu utalii na kupanga madaraja ya watendaji.

“Kazi hizi ni kazi za msingi za Bodi ya Utalii na siyo wizara. Hata hivyo, idara hiyo katika bajeti ya awali ilikuwa imetengwa kiasi cha shilingi bilioni 2.55 kama OC (matumizi mengineyo), kiasi ambacho kwa maoni ya kamati kinatosha kufanya shughuli hizo,” alisema Mnzava.

Aliongeza kuwa katika nyongeza hiyo shilingi bilioni 2 zimeelekezwa katika ujenzi wa mifumo ya Tehama ujulikanao

Habari

Bunge lagomea bajeti ya ziada utalii

Inatoka Uk. 13

kwa jina la Tanzania Safari Booking Platform, lakini kamati imebaini kwamba wakati fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji mradi huo, hauna andiko la awali wala gharama zake halisi.

“Pamoja na manufaa yanayotarajiwa ya mfumo huo, maandalizi ya utekelezaji hayajafanyika, hivyo fedha hizi zinaweza kutumika vibaya,” alisisitiza.

Aidha, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali (DDMCC), kuna sehemu ya mfumo wa kufanya miadi (booking) na kuwaunganisha watalii kutoka nje ya nchi na huduma za hoteli na usafiri ijulikanayo kama Travel Companion.

Mnzava alisema kujenga mfumo kama huo ndani ya wizara hiyo ni matumizi mabaya ya fedha za umma kwani kitu kama hicho tayari kipo katika taasisi iliyo chini ya wizara hiyohiyo.

Mnzava aliliambia Bunge kuwa kitu kibaya zaidi ni kuwa serikali ilionekana kuihadaa kamati hiyo, huku akifafanua kwamba baada ya kamati kutokubaliana na matumizi ya nyongeza, ilitoa siku 15 kwa serikali kufanya marekibisho na serikali ikakubali kufanya hiyo.

“Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kuwa kikao kilichofanyika tarehe 21 Mei, 2024 ili kupokea utekelezaji wa mapendekezo ya kamati, ilitaarifiwa kwamba mabadiliko hayawezi kufanyika kwa sababu vitabu vimefungwa jambo ambalo siyo sahihi...

“... Mchakato wa ufungaji wa vitabu vya bajeti unafanyika baada ya kupitisha Sheria ya Matumizi,” alisema Mnzava na kushangaa kwani serikali haikuwa na msimamo wa kweli!

Msimamo huo wa kamati kugomea bajeti ya ziada uliungwa mkono na wabunge kadhaa waliochangia bajeti hiyo akiwamo Ester Bulaya ambaye aliutaja



Watalii wakiwa maeneo ya vivutio vya Tanzania

mpango huo wa matumizi ya bejetei ya zaidi ni wa kifisadi na anasa.

“Kazi iliyofanywa na kamati ni kazi ya kibunge, ni kazi iliyotukuka. Imetusaidia kazi sisi wabunge, na sisi kama wabunge tunapaswa kuiheshimisha Kamati na Maliasili na Utalii,” alisema Bulaya.

Aliwahimiza wabunge wenzake kutoyapitisha maombi hayo ya bajeti ya ziada kwa sababu kiasi kikubwa cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kuwanufaisha watendaji badala ya kushughulikia matatizo ya msingi ndani ya wizara.

“Bunge tusikubali kuyapitisha maombi haya. Maombi ya matumizi mabaya ya fedha za umma, maombi ya kifisadi, maombi ya anasa,” alisema.

“Mnatuletea maombi kama haya wakati juzi hapa tumetoka kwenye bajeti ya maji mmepunguza fedha za wananchi kupata maji. Jana hapa bajeti ya ujenzi ilikuwa hatari, barabara zimeharibika huko, wananchi wanashindwa kupita, halafu mnataka Bunge tupitishwe anasa hizi, hapana...

“... Hizi ni fedha za walipa kodi zitalindwa ili zikafanye kazi ya kuwaendeleza wananchi wetu,” alisisitiza.

Mjadala wa bajeti ya wizara hiyo unatarajiwa kuhitimishwa leo - Jumatatu.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Uchambuzi

Ziara kusikiliza kero uthibitisho mifumo imekufa

Na Mwandishi WETU

NI dhahiri kwamba mifumo ya kuhudumia wananchi katika Tanzania, imekufa.

Hakuna kinachoonekana kwenda sawasawa kwani wanaopaswa kutenda, wameamua ama kususa, au hawajui wajibu wao na huenda pia ni wazembe.

Ni kama bila ziara, hasa za wanasiasa, wananchi wanakosa huduma na kubaki kushangaa serikali yao inafanya nini.

Alianza Paulo Makonda kupita nchi nzima akitoa uamuzi wa kuonyesha ombwe la watendaji wa serikali katika kutatua kero na changamoto za wananchi.

Hakika Makonda, pamoja na upungufu kadhaa katika kuchukua hatua, aliweza kuonyesha wapi kuna matundu katika utendaji wa serikali.

Sasa karibu kila kiongozi anajitahidi kufanya ziara za vijijini kusikiliza kero za wananchi. Hali hii inatokana na agizo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye katika moja ya hotuba zake alieleza kufurahishwa jinsi Makonda, wakati akiwa Katibu wa Uenezi na Itikadi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alivyokuwa anasikiliza na kutatua kero za wananchi.

Samia akashangaa kwa nini viongozi wengine hawaigi mtindo huo na wao kuanza kusikiliza na kutatua kero za wananchi kama alivyokuwa akifanya Makonda!

Katika hotuba nyingine Rais Samia akasema waziwazi kuwa anghenda kuona viongozi katika ngazi zote wakishuka kwa wananchi na kusikiliza kero zao na yeye binafsi atafuatilia ziara

hizo.

Muda mfupi baada ya hapo ndipo tukaanza kushuhudia viongozi katika ngazi mbalimbali wakipanga ziara rasmi za kuzunguka vijijini kwa lengo la kwenda kuwasikiliza wananchi wenye shida.

Na sasa nchi 'imechafuka' kwa ziara hizi za viongozi kwenda kwa wananchi kusikiliza kero. Kila kiongozi yuko 'site' akisikiliza na kutatua kero.

Lakini inavyoolekea, huu utaratibu hautasaidia sana kupatia ufumbuzi kero na shida nyingi za wananchi.

Kwanza, hautoi suluhu la kudumu la utatuzi wa kero zinazowakabili wananchi. Kwa kiasi kikubwa utaratibu huu unajikita katika kutatua kero za mtu mmoja mmoja.

Sasa endapo kero au shida hiyo imetokana na kufeli kwa mfumo, basi ni dhahiri kuwa kesho atatokea mtu mwingine atakayepatwa na shida kama hii ambayo kiongozi anaitatua leo.

Hivyo, wakati kiongozi akimaliza kusikiliza kero za wananchi, atajikuta nyuma yake akiwa na msururu wa watu



Paulo Makonda akielekea kwenye mkutano tayari kusikiliza kero za wananchi na pengine kufanya uamuzi ambao unapaswa kufumbuliwa na mifumo. (Picha: CCM)

Ziara kusikiliza kero uthibitisho mifumo imekufa

Inatoka Uk. 16

wengine wanya wenye kero kama zile ambazo alishazitaua kwa waliotangulia.

Hii inatokana na sababu moja kubwa, kwamba mifumo iliyopo haitatui kero hizo, hivyo ni dhahiri kuwa wenye kero wataendelea kuzaliwa kila leo.

Hivyo, kiongozi atajikuta hana muda wa kufanya kitu kingine zaidi ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Pili, kwa kiasi kikubwa kuna uwezekano wa kuonea watu maana mara nyingi kero hizi husikilizwa upande mmoja tu.

Kawaida wakati wa kusikiliza kero hizi aghalabu yule mwenye tatizo ndiye anakuwepo kuelezea tatizo lake na anayetuhumiwa hayupo.

Katika mazingira kadhaa, wengi wa wahusika katika kero hizo hawapo wakati ule kero inaposikilizwa naye akiwa mtuhumiwa.

Kwa kuwa kiongozi anakuwa amejipanga kutoa suluhu kuhusu kero hizo, basi mara nyingi suluhu hutolewa kwa kusikiliza upande mmoja tu kuhusiana na kero huisika.

Tatu, kuna kuingilia kwingi kwa mamlaka nyingine katika usikilizaji wa kero. Tumeshuhudia kero nyingi zikihusu masuala yaliyoko mahakamani.

Wapo baadhi ya viongozi wenye viburi ambao huendelea kusikiliza kero za aina hiyo na kuzitolea uamuzi papo kwa hapo. Huku ni kuingilia mamlaka ya taasisi nyingine zinazohusika na utataji wa kero kisheria.

Hata pale ambapo hukumu inakuwa imetolewa kuna utaratibu unaotakiwa



Wasiri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (kushoto) akisikiliza kero za wananchi na kutoa uamuzi. (Picha kutoka wizarani).

ufuate wa kimahakama kuhakikisha kuwa yule aliyeshinda anapewa haki yake, siyo tu kwa amri au agizo la kiongozi.

Katibu wa Uenezi na Itikadi mpya wa CCM, Amos Makalla alibaini kuwa hili ni tatizo na akatangaza kuwa katika usikilizaji wa kero, CCM haitajihusisha na masuala ambayo yako mahakamani.

Teleweke kuwa wananchi kukimbilia kwa wanasiasa ili watatuliwe kero zao, ni uthibitisho kuwa mifumo iliyowekwa ili kuhakikisha matatizo ya wananchi yanatatuliwa imeshindwa kufanya kazi.

Na siyo tu kuwa imeshindwa kufanya kazi, bali pia wananchi ni kama wameshindwa kuiamini mifumo hiyo rasmi.

Upo uwezekano kuwa mifumo imeshindwa kufanya kazi kutokana na ubovu au udhaifu wa mifumo hiyo. Pia upo uwezekano kuwa mifumo imeshindwa kufanya kazi kwa sababu binadamu ameifanya ishindwe kufanya kazi kwa malengo mbalimbali.

Malengo hayo mengi binafsi ambayo yanatoa mwanya wa kupata kipato haramu, lakini pia huenda ni watendaji

Uchambuzi

Ziara kusikiliza kero uthibitisho mifumo imekufa

Inatoka Uk. 17

kushindwa kufahamu jinsi ya kuifanya mifumo iliyopo ifanye kazi sawasawa.

Kinachoendelea sasa hivi kwa viongozi kutoka na kuanza kusikiliza kero ni uthibitisho kuwa hatuiamini tena mifumo katika uwezo wake wa kutatua matatizo yanayokabili wananchi.

Kama wananchi wangukuwa bado wanaiamini mifumo hiyo, ni dhahiri kuwa wengi wangejiuliza ni kwa nini haifanyi kazi na kutafuta suluhu ili iweze kufanya kazi zilizokusudiwa.

Katika mazingira ya sasa, wananchi wamekata tamaa na mifumo iliyopo na

Ieleweke kuwa utaratibu wa viongozi binafsi kugeuka mfumo, una udhaifu mwingi,

wanaamini zaidi katika viongozi kutatua kero za mtu mmoja mmoja.

Ieleweke kuwa utaratibu wa viongozi binafsi kugeuka mfumo, una udhaifu mwingi, na hakika unapaswa kuangaliwa vyema ili kuepusha kila kiongozi, hasa wa kisiasa, kuwa mfumo binafsi.

Kinachofanyika kwa kila kiongozi kuwa mfumo, ni kutibu matokeo ya tatizo badala ya kutafuta kiini cha tatizo.

Ni kweli kuwa kuna kero nyingi sana katika jamii zikiwakabili mtu mmoja mmoja. Kama liyobainisha awali, hali hiyo ni matokeo ya mifumo kushindwa kufanya kazi.

Katika mazingira ya mifumo kushindwa kufanya kazi, serikali ingeonkana inawajibika zaidi endapo ingekuja na majawabu ya kwa nini mifumo hiyo imeshindwa hadi kusababisha wananchi



Wasiri Mkuu Kassim Majaliwa akihutubia. Huyu ni nadra sana kutoa uamuzi ambao unahitaji mifumo kuamua tofauti na wengi wa wasaidizi wake (Picha: Global Publishers)

kukimbilia kwa wanasiasa wenye uamuzi wa “chap-chap” hata kama una madhara makubwa baadaye.

Endapo ingefahamika kwa nini mifumo ya kutatua kero za wananchi imekufa, serikali ingetafuta namna nzuri ya kurekebisha na kuamua kuirejesha ili iwe rahisi kwa wananchi kupata ufumbuzi wa kero na shida zao.

Mifumo ikifanya kazi vyema, hakuna sababu ya viongozi kushinda siku kadhaa, tena eneo moja wakisikiliza shida za mtu mmoja mmoja.

Mathalan, wananchi wameshuhudia watu wengi wakienda kwa viongozi wakiwa na kero kuhusiana na masuala ya ardhi. Wengine wameondolewa kwenye viwanja vyao, wengine wamedhulumiwa viwanja vyao, wengine wamevamiwa katika viwanja vyao na kadhalika.

Katika hili inatakiwa tu kuitumia vyema mifumo iliyoweka ili kuhakikisha masuala ya ardhi yanaendeshwa kisayansi. Na hapa lazima ingebainika matatizo yako wapi na kupatiwa ufumbuzi wa uhakika na yenye kuegemea sheria na taratibu.

Polisi acheni kupiga ramli

Mhariri,

NAANDIKA barua hii kwa niaba ya makuruta tuliofukuzwa kutoka Jeshi la Polisi tukiwa bado mafunzoni.

Kupitia kwako, ninaamini wakuu wa jeshi hilo na viongozi wengine, hasa Wizara ya Mambo ya Ndani watasikiliza kilio chetu na ikiwezekana kuchukua hatua ili kukomesha unyanyasaji na kudhalilishwa kwa utu.

Makututa kadhaa tulifukuzwa kwa sababu ya tuhuma kwamba tuna vidole virefu na makalio makubwa hivyo kudhaniwa kuwa ni "mashoga."

Napenda ifahamike kwamba vidole na viuno vyetu siyo vikubwa kama ilivyotangazwa. Na kama ingekuwa hivyo, jeshi lilipaswa kuchukua vipimo vya kisayansi na kitabibu ili kuthibitisha tuhuma zao kwetu, lakini hilo halikufanyika kamwe.

Uongozi wa jeshi hilo haukuchukua vipimo vya aina yoyote, isipokuwa kubebwa na hisia.

Hivyo, kufanya uamuzi kwa pupa kwa kutumia makisio ya kienyeji kama wapiga ramli wazushi; kwamba wenye vidole virefu na makalio makubwa, ni mashoga.

Wakubwa hawa wa jeshi wametumia sayansi batili ya zama za mawe wakati sayansi mamboleo zipo.

Kutokana na kuonewa, kudhalilishwa na kutwezwa utu wetu, tunaomba serikali, kupitia wizara husika kurudisha makuruta wote waliofukuzwa kwa tuhuma tu.

Ikiwezekana kabla ya kurudishwa, vipimo vya makuruta wote vichukuliwe na ukweli kwamba nani shoga na yupi siyo, ufahamike kisayansi.

Aliyeonewa,
Dodoma.

Dawa za kisukari adimu

Mhariri,

KUMEKUWEPO upungufu mkubwa wa dawa za magonjwa yasiyoambukiza, hasa kisukari katika hospitali nyingi nchini.

Mimi ni miongoni mwa wagonjwa wa kisukari ambao tumekuwa tukihudumiwa na serikali kwa kupatiwa dawa za kutuliza makali ya ugonjwa huo, lakini kwa sasa hazipo ama zipo kwa kiasi kidogo katika hospitali nyingi.

Hali hiyo nimeithibitisha katika hospitali ya Mwananyamala, Dar es Salaam, Sekou Toure, Mwanza na Bombo, Tanga. Kote huko nimetembelea hivi karibuni kwani shughuli zangu zinanipa fursa ya kufika maeneo mengi.

Mara nyingi ukifika dirishani kwenda kupata dawa, unaelezwa na wahusika kwamba hakuna dawa, sababu kubwa wakieleza kwamba hawajapokea kutoka serikalini.

Sasa najiuliza, hivi hii serikali imegoma kuagiza dawa za wagonjwa kisukari? Je, kwanini iwe hivyo sasa au kuna mambo ya hovyoyanaendelea?

Naomba serikali ifuatilie hili na ihakikishe dawa za magonjwa yasiyoambukizwa, hasa kwa sisi wazee, zinapatikana kwa wingi, katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Athumani Lugelo,
Kinondoni,
Dar es Salaam.

Tunapokea Barua

Mhariri anapokea barua kutoka kwa wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@tampa.or.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263

Makala

Sheria mpya ya habari Z'bar ipitishwe sasa

Na Hamis Mzee

BADO Serikali ya Mapinduzi Zanzibar binaonekana kusuasua kuhakikisha kunakuwepo sheria mpya ya habari.

Kuendelea kuchelewa kupatikana kwa sheria hiyo mpya, kunaminy haki kubwa ya wananchi wa visiwa hivyo, kufurahia uhuru mpana wa kuhabarishwa na wakati huo huo, waandishi wa habari wanakosa mazingira mazuri ya kufanya kazi zao.

Mwaka huu ni kipindi kingine tena wadau wa habari wa Zanzibar wanaendelea kuhimiza kutungwa kwa sheria mpya ya habari.

Safari hii katika kuadhimisha Siku ya Uhuru Vyombo vya Habari Duniani huko Zanzibar, Katibu Mtendaji wa Baraza Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura, ametoa mwito kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuharakisha kutungwa na kupitishwa kwa sheria hiyo.

MCT imekuwa ikishirikiana na wadau wa habari Zanzibar katika mchakato wa kupata sheria ya habari iliyoboreshwa kwa muda mrefu, lakini hadi sasa kuna mkwamo unaoelezwa kuwemo ndani ya baadhi ya ofisi za watendaji wa serikali.

Licha ya kuwepo matumaini ya kupatikana sheria hiyo, kumekuwa na kusuasua katika ukamilishaji wake.

Kwa wadau wenye uzoefu wa masuala ya habari katika hatua za awali, ilionekana kuwa Zanzibar ingekuwa ya kwanza kupata sheria hiyo kabla ya Tanzania Bara.

Hata hivyo, Tanzania Bara baada ya mchakato uliodumu kwa zaidi ya miongo miwili, hatimaye Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari (MSA) na nyingine ya Haki ya Kupata Taarifa (ATI), zilipitishwa 2016, ikiiacha Zanzibar.

Wakati MSA tayari imefanyiwa hadi marekebisha na Bunge kuondoa vipengele hasi, bado Zanzibar inaelewa kuwa katika hatua ya utungaji wa sheria hiyo.



Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi

Ingawa suala la habari siyo suala la Muungano, wakati mmoja akifungua mkutano wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) uliofanyika Zanzibar, Rais Dkt. Hussein Mwinyi aliwahimiza mawaziri wa habari wa pande hizi mbili; Nape Nnauye wa Serikali ya Muungano na Tabia Mwita wa Zanzibar, kushirikiana kufanikisha sheria ya habari ya Zanzibar.

Katika mkutano huo wa TEF, ilitahadharishwa kwamba siyo vyema kwa sheria hiyo ya Zanzibar kulingana na ile ya Tanzania Bara, kwani wakati huo kulikuwa na mchakato wa kurekebisha vipengele hasi.

Wadau wa habari Zanzibar wamekuwa wakihimiza kupitishwa kwa sheria mpya kwa lengo la kuboresha utendaji kazi kwa waandishi wa habari kulingana na mazingira ya sasa.

Mchakato wa wadau wa habari Zanzibar unalenga kufuta Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu Namba 5 ya mwaka 1988 na kutungwa Sheria ya Huduma ya Habari na mambo yanayohusiana nayo.

Ni vyema sasa wenye mamlaka Zanzibar, kusikia kilio cha wadau ili kufanikisha kupitishwa sheria hiyo haraka.

Je, ANC sasa imejiandaa kisaikolojia?

Na Mwandishi WETU

DALILI zilishaanza kujitokea - miaka kadhaa iliyopita kwamba chama tawala nchini Afrika Kusini, African National Congress (ANC), kinaelekea mwisho wake.

Ingawa kuna watu hawakubali hilo, lakini matokeo ya uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita umedhihirisha kuwa mwisho wa chama hicho tayari umeshaanza.

Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka takribani 30 tangu kiingie madarakani, chama hicho kimeshindwa kupata zaidi ya nusu ya wabunge katika Bunge la Taifa ili kuwa na uhuru na haki ya kuunda serikali bila ya kushirikisha vyama vingine kama ambavyo imekuwa ikifanya miaka yote.

Matokeo ya Uchaguzi Mkuu yanaonyesha kuwa chama hicho kinaelekea kupata chini ya asilimia 40 na hakiwezi tena kuunda serikali peke yake.

ANC kitabakia madarakani iwapo tu kitafikia makubaliano ya kuungana na chama au vyama vingine ili kupata idadi ya wabunge inayotakiwa na sheria kwa vyama hivyo kuunda serikali. Chama kinatakiwa kupata zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya wabunge 400.

Kuungana ili kupata idadi hiyo ni mtihani mzito kwa ANC.

Kwa hesabu ya haraka, ANC, ambayo inakadiriwa kupata asilimia takribani 40 ya viti bungeni, ingeweza kuungana na Democratic Alliance (DA), ambayo inaweza kupata hadi asilimia 20 ya wabunge.

Ikiwa vitakubaliana, kwa pamoja vyama hivyo vinaweza kuwa na idadi ya wabunge inayokaribia asilimia 60, lakini mchakato wa vyama hivyo kuungana na mgumu sana.

Kuelekea mwishoni mwa wiki, lilitolewa pendekezo la ANC kuungana



Rais Ramaphosa akipiga kura wiki iliyopita

na DA, chama ambacho kilianzishwa kikiwaleta pamoja wazungu na Waafrika baada ya kukomeshwa kwa siasa za ubaguzi wa rangi nchini humo.

Kuundwa kwa chama hicho ilikuwa ni kama mwiba kwa ANC kwani kilipoteza baadhi ya wanachama wake ambao waliamua kujiondoa na kujiunga na DA.

Hivyo, kwa miaka mingi ANC imekuwa ikichukulia DA kuwa ni hasimu wake namba moja miongoni mwa vyama vote vya siasa ndani ya Afrika Kusini.

Hivyo, linapokuja wazo la vyama hivyo kuungana kuna baadhi ya viongozi na wanachama, hasa wahafidhina ndani ya ANC ambao hawataki kabisa kulisikia pendekezo hilo.

Wao wanasema kamwe hawawezi kuungana na chama hasimu ambacho ni sehemu ya anguko la ANC. Mwishoni mwa wiki baadhi ya viongozi wa ANC walitishia kujiuzulu nafasi zao iwapo chama chao kitaungana na DA ili kuunda serikali ya mseto.

Ugumu wa ANC kuungana na vyama vingine hauishii tu kwa DA. Vyama ambavyo vinaweza kuungana na ANC na kuunda serikali ni pamoja na uMkoto weSiwe (MK) cha Jacob Zuma na

Afrika Kusini

Je, ANC sasa imejiandaa kisaikolojia?

Inatoka Uk. 21

Economic Freedom Fighter (EFF) cha Julius Malema.

Lakini, hao wote wameunda vyama vya baada ya kujiondoa ANC na hilo limetengeneza uhasama mkubwa baina yao. Hivyo, uwezekano wa ANC kuunga a na MK au EFF ni mdogo.

Zuma alikiunda MK mwishoni mwa mwaka jana na baada ya miezi sita tu kimefanikiwa kupunguza idadi ya kura za ANC.

Kwa kiasi kikubwa chama hicho kimezoa kura nyingi katika jimbo la Kwa Zulu Natal, nyumbani wa Zuma.

Hata hivyo, hadi sasa bado Zuma anajitangaza kuwa mwanachama wa ANC, huku akiendesha chama kingine ambacho kimeinyang'anya ANC kura na hilo limewaudhi watu wengi ndani ya ANC ambayo juhudi zake za kutaka MK isisajiliwe ziligonga mwamba ingawa ilifanikiwa katika kesi ya kumzuia Zuma kuwania ubunge.

Wazo la vyama hivi kuungana linatokana na makadirio kuwa MK inaweza kupata asilimia 14 ya viti bungeni na hivyo iwapo ikiungana na ANC vyama hivyo vinaweza kuwa na idadi ya wabunge watakaovivezesha kuunda serikali.

Kwa upande wa EFF, misimamo mikali ya Julius Malema ni jambo ambalo linakifanya siyo tu ANC, bali chama kingine chochote, kuwa na woga wa kuungana nacho kuunda serikali ya mseto.

Ukiacha serikali ambayo itajumuisha ANC ni vigumu zaidi kuwa na serikali ambayo haitakuwa na ANC. Hii ni kwa sababu uhasama uliopo baina ya vyama vya upinzani unafanya vigumu kwa vyama hivyo kuungana.

Ifahamike kuwa kwa upande wa upinzani, kutokana na kugawana kura kuna mlima mrefu kwa wao kufikia idadi



Jacob Zuma

ya wabunge itakayovivezesha kuunda asderikali.

Kuna takriban vyama 70 vya upinzani na wogombea binafsi kama 10 hivi.

Vyama vikubwa vya upinzani ni pamoja na DA (ambayo hadi jana ilikuwa na asilimia 20 ya kura), MK (asilimia 14), EFF (asilimia 9) na Inkatha Freedom Party (IFP) ambayo inaweza kupata asilimia nne. Vyote hivi vikiamua kuungana bado havitafikisha idadi inayotakiwa kuunda serikali.

Hivyo, ili kuungana vitahitaji vyama vingine vidogo kuungana navyo. Hii ni kazi ngumu sana hasa ukizingatia aina ya siasa ambazo zinatawala demokrasia ya Afrika Kusini.

Kilichoanguisha ANC

Anguko la ANC halikuanza hivi karibuni. Ni kama maandishi ambayo yalikuwapo ukutani, lakini wahusika walishindwa kuyaelewa au waliyaelewa na upepo wa mabadiliko ukawazidi nguvu.

Anguko la ANC lilianza na harakati za kumuondoa madarakani aliyewahi kuwa Rais wa Afrika Kusini, Thabo Mbeki mwaka 2008, huku chanzo kikiwa ni Jacob Zuma ambaye mwaka mmoja

Je, ANC sasa imejiandaa kisaikolojia?

Inatoka Uk. 22

baadaye alichaguliwa kuwa kiongozi wa ANC akimshinda Mbeki katika uchaguzi mkali sana.

Mbeki alimwondoa Zuma kuwa makamu wake wa rais mwaka 2005 kutokana na kesi za rushwa zilizokuwa zikimkabili Zuma na uhasama ukaanzia hapo.

Inaelezwa kuwa Zuma alikuwa nyuma ya harakati za kumwondoa Mbeki kwenye nafasi ya urais na alipoondoka alirithiwa na Kgalema Matlanthe akiwa rais wa mpito kabla Zuma hajaingia madarakani baada ya kushinda uchaguzi uliofuatia.

ANC ikazidi kugawanyika zaidi chini ya Zuma. Na kama Waswahili wasemavyo - ukiuma kwa upanga na wewe utauawa kwa upanga, alichokifanya Zuma kwa Mbeki kikamkumba na yeye kwani aliondolewa madakani na nafasi yake kuchukuliwa na rais wa sasa, Cyril Ramaphosa.

Lakini Zuma alipoondolewa hakukubali kirahisi kama ilivyokuwa kwa Mbeki ambaye aliamua kuachana kabisa na masuala ya siasa na kujikita kwenye mambo mengine.

Zuma aliendelea kulumbana na wanasiasa ndani ya ANC akiamini kuwa walimwondoa madarakani kwa hila. Katika malumbano hayo, akajikuta akikabiliwa na kesi za mbalimbali zikiwamo za rushwa na matumizi mabaya ya ofisi.

Katika moja ya kesi hizo alihukumwiwa kifungo cha miezi 15 gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kudharau mahakama na hukumu hiyo ndiyo imemfanya ashindwe kuwania ubunge kwenye uchaguzi huu.

Ukiangalia jinsi Zuma anavyoendesha saisa zake, ni dhahiri kuwa bado ana chuki kubwa dhidi ya baadhi ya wanasiasa na hasa dhidi ya chama "chake cha zamani" cha ANC.



Julius Malema

Uhasama huo unazidi kukididimzia zaidi ANC kwani nguvu alizo nazo Zuma siyo za kubeza. Zuma anakijua ANC kwa undani, hivyo ni rahisi sana kwake kukufanyia hujuma za wazi na za kificho.

Inaaminika kuwa hata kashikashi za kiasiasa na kisheria ambazo Rais Ramaphosa anakumbana nazo katika miaka ya hivi karibuni, zina mkono wa Zuma nyuma yake.

Kwa namna yoyote ile ANC haiwezi kuwa salama Zuma akiwa nje ya chama hicho, kwani ataendelea kukisakama kwa lengo ya kukidhoofisha.

Lakini kwa upande mwingine, ANC haiwezi pia kuwa salama Zuma akiwa ndani yake kwani uhasama wake na wanasiasa ambao bado wapo ndani ya ANC, utaleta migawanyiko mikubwa itakayotishia uimara wa chama hicho.

Kwa sasa hivi ANC ni chama kinachoweza kueleza kuwa kiko katika mtari mwembamba wa uhai wake na anguko lake kwa wakati huohu.

Kazi kubwa kwa sasa ni kwa chama hicho kuangalia wapi kinaweza kuimarika tena, hasa kwa kuaminiwa na kundi kubwa la vijana.

Pongezi kwa kamanda...



Askari akisaidia kufunga gidamu za mtoto kabla ya kuruhusu binti huyo na wenzake kuvuka barabara. Picha hii iliyochotwa kwenye mtandao, haina maelezo ya kutosha, lakini inaelewa kuwa ilipigwa jijini Arusha na kwamba jina la askari huyo halikupatikana. Endapo kuna mwenye taarifa zaidi, gazeti la Pambazuko lingependa kupata kupitia namba hii: 0744 768 263.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.